

MAONO YA WILLIAM BRANHAM



Kanda hii inatengenezwa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, nipoiwasilisha kwa Ndugu Lee Vayle kwa ajili ya muswada wa kitabu. Ndugu Vayle ameniuliza, hapa mbele za Ndugu Mercier, ku—kutaja baadhi ya maono yaliyopita. Bila shaka, maono ambapo kama . . . mimi . . . ya kwa- . . . Moja ya mambo ya kwanza ninayokumbuka, ni maono, yakija. Maono huja wakati wote. Lakini baada ya kuongoka kwangu ndipo ninafikiri ndipo mliokuwa na shauku napo, Ndugu Vayle.

² Vema, ninakumbuka, baada ya kutawazwa kanisani, kanisa la Kibaptisti, na Dk. Roy Davis, hapa kwenye Barabara ya Watt huko Jeffersonville ambapo kanisa lilikuwa wakati huo. Ninakumbuka ono moja la kipekee, si zaidi ya majuma machache baada ya ninii yangu . . . yapata . . . ningesema, siku chache baada ya kutawazwa kwangu. Nilikuwa . . . niliona ono la mwanamume mkongwe aliyekuwa amelala hospitalini, ambaye alikuwa amepondwa. Alikuwa ni mtu mweusi. Naye akaponywa mara moja, kiasi kwamba, hata ilisababisha utata mwingi. Naye akaamka kutoka kitandani na kuondoka akitembea.

³ Basi siku mbili, yapata siku mbili, baadaye, nilikuwa nikikata huduma, huduma ambazo hazijalipiwa huko New Albany, maji, na gesi, na—na bili za stima. Na hiyo . . . Nilijawa sana na furaha! Kila mara ningepata nyumba ya kale, ningeingia tu na kuomba, mwajua, ambapo hapakuishi mtu.

⁴ Na ninakumbuka kumwambia Bw. Johnny Potts, ambaye angali hai leo. Yuko karibu sana, nadhani, kufikisha umri wa miaka sabini ama themanini. Alikuwa ni mzee msoma mita. Nao walikuwa wamemtoa katika usomaji mita wakati huo, na walikuwa wamemweka kwenye dawati, kupokea malalamiko na kadhalika, ulipoingia mlangoni, na simu za huduma. Nami nilikuwa nikimwambia kile Bwana alichokuwa amenionyesha. Naye alikuwa, mara moja moja, akichukua mita chache zilizopitwa ambazo mtu wa kawaida hakuona. Na katika hili, a—alikuwa akisema, mtu . . .

⁵ Ambalo, nilikuwa nimeliona kwenye gazeti, ambapo walikuwa na behewa chakavu . . . Katika siku hizo, waliendesha farasi wawili, nao wakaokota uchafu na takataka, kichochoroni. Kulikuwa na maskini mtu mweusi jina lake Bw. Edward J. Merrell. Aliishi kwenye Barabara ya 1020 huko New Albany. Naye alikuwa amegongwa na wazungu wawili, ambao walikuwa ni msichana wa kizungu na—na mvulana, wakiendesha motokaa. Naye alikuwa amepoteza udhibiti wa hiyo motokaa, na alikuwa amemponda kwenye gurudumu la mkokoteni. Na hilo likavunja kabisa mifupa yote mwilini mwake, karibu hivyo, na iliyo

kwenye sehemu ya kifua chake, sana sana. Likagonga na kuumbua kabisa mgongo wake. Nao wakampeleka hospitalini, mahututi.

⁶ Ndipo Bw. Potts, akipitia ho—hospitali kule New Albany, alikuwa amemwambia kuhusu Bwana kuhusika nami. Basi akaagizia nije, nimwombee. Ndipo ghafla, nikawaza, “Huyo ndiye mtu ambaye nimemwona katika ono hili.”

⁷ Kwa hiyo, ki—kidogo niliogopa kwenda, maana hiyo ilikuwa ni mojawapo ya yangu ya kwanza, mnaona, kwenda namna hiyo. Kwa hiyo, lakini, hata hivyo, nilienda na kumchukua rafiki yangu, ambaye alikuwa ndiyo kwanza aongoke, maskini mvulana wa Kifaransa jina lake George DeArk. Nami nilikuwa ndiyo kwanza nimwongoze kwa Kristo. Basi tukapanda juu. Nami nikasema, “Sasa, Ndugu George, ni—ni—ninataka ukumbuke. Mambo haya yanayonitendeka, siwezi kuyaelewa. Lakini, kumbuka, mtu huyu atapona. Na akipona, kuna... Siwezi kumwombea mpaka hao wazungu wawili waje na kusimama upande huo mwingine wa kitanda, maana inanibidi kuifanya jinsi nilivyoonyeshwa.”

⁸ Ndipo nikaenda ho—hospitalini na kuulizia Bw. Merrell. Basi nikaenda pale, naye mke wake akaniambia alikuwa katika hali mbaya sana. Na asingeweza kusogea kwa sababu kwamba eksirei zilikuwa zimeonyesha kwamba baadhi ya hii mifupa ilikuwa karibu sana na pafu. Basi iwapo angesogea, mbona, ingeweza, huenda ikatoboa mapafu yake na kumfanya atokwe damu hata kufa. Naye alikuwa katika hali mbaya sana. Pia kulikuwa kunatoka damu kidogo kutoka kooni mwake, na kadhalika, kwa sababu alikuwa anatokwa damu sehemu ya kinywa. Alikuwa amekaa hapo yapata siku mbili. Naye mtu huyo alikuwa, wakati huo, alikuwa na yapata umri wa miaka sitini na mitano, nadhani, sitini ama sitini na mitano. Mtu mkongwe; masharubu yake, marefu, yamekuwa meupe. Nazo nywele zake zilikuwa na mvi.

⁹ Basi niliingia na kumwelezea mtu huyu, hata hivyo, ono nililokuwa nimeona kutoka kwa Bwana. Ndipo wale vijana wakaingia, waliokuwa wamemgonga. Nami nikapiga magoti niweze kumwombea. Ndipo mara ghafla, mtu huyu akapiga mayowe, akisema, “Nimepona,” na kuruka. Naye mke wake, akijaribu kumshikilia, kitandani. Ndipo mmoja wa madaktari walio mazoezini akaja, akijaribu kumshikilia kitandani. Ndipo akaruka kutoka kitandani, akaleta msisimko mwingi. Basi nilipoenda kwenye... Nikamwambia Ndugu George...

¹⁰ Halafu mmoja wa masista, ilikuwa ni hospitali ya Katoliki, akaja na kusema ilibidi nitoke humo, hivyo kumfanya mtu huyo asisimkwe. Maana, alikuwa na joto la homa, yapata mia moja na nne. Na jambo la kushangaza, walipomrudisha ndani; ka—kasisi, mahali hapo, na baadhi ya madaktari walipokuwa wamemweka,

wakamfanya arudi kitandani, kwa kuwa alikuwa anavaa nguo zake. Basi walipompima halijoto, hakuwa na joto la homa.

¹¹ Sasa, wapo watu wengi walio hai leo, ambao waliona ono hilo, waliliona likitukia, ama wanajua habari zake.

¹² Basi nikatoka nje na kusimama kwenye vipandio, nikamwambia Ndugu George, “Sasa, angalia. Atakuwa amevaa koti la hudhurungi na kofia ya kitambaa. Atashuka moja kwa moja akitembea kwenye vipandio hivi, katika dakika chache.” Na hakika alishuka. Alitokea moja kwa moja na kushuka akitembea.

¹³ Basi yapata u—u—usiku mmoja baadaye, Bwana akanitokea tena, asubuhi moja, karibu kwenye mapambazuko, na kunionyesha mwanamke aliyelemaa vibaya, ambaye alikuwa anaenda kuponywa. Kwa hiyo nikasema, “Vema, labda—labda nitajua mahali alipo.”

¹⁴ Na kwa hiyo nikateremka chini na nilikuwa nikifungulia maji, juu ya, ninaamini ilikuwa, karibu na Barabara ya Nane huko New Albany. Na nilikuwa na... Ilikuwa ni makao ya nyumba mbili, nami nilihofia nilikuwa nimefunga pande zote mbili. Upande mmoja, watu walikuwa wamehama; na upande huo mwingine, kulikuwa na watu. Kwa hiyo nikaenda upande huo mwingine ambao ulikuwa na wa—watu, iliyokaliwa. Basi nikabisha mlangoni. Nao walikuwa wa—wa—watu maskini kabisa. Ndipo msichana mdogo mwenye sura ya kuvutia sana, akaja mlangoni, huku amevalia kifukara. Na yeye—yeye akasema, “Wataka nini?”

Nikasema, “Unaweza kujaribu maji, uone kama yamefungwa?”

¹⁵ Naye akasema, “Naam, bwana.” Na akaenda. Akasema, “La. Maji hayajafungwa.”

Nikasema, “Asante.”

¹⁶ Naye mama yake, amelala kitandani, jina lake ni Bibi Mary Der Ohanian. Naye alikuwa ni Mwarmenia. Mvulana wake alikuwa akicheza beki, ninaamini ndivyo ilivyokuwa, katika difensi ya New Albany, timu ya kandanda. Naye msichana, binti yake, alikuwa katika shule ya sekondari ya juu. Jina lake lilikuwa ni Dorothy. Ndipo akasema... Dorothy akaniambia, “Hivi wewe si yule mtu wa Mungu aliyekuwa na ule uponyaji hapa hospitalini, hivi majuzi? Mama yangu angependa kuzungumza na wewe.” Nami nikaingia.

¹⁷ Basi akaniambia kwamba alikuwa amelala, kiwete. Na alikuwa amelemaa, kitandani, miaka kumi na saba, tangu alipozaliwa msichana huyu. Na kwa hiyo msichana huyo alikuwa na umri wa miaka kumi na saba. Kwa hiyo basi nikamwambia ya kwamba... Akasema, “Hivi wewe ndiwe yule mtu wa Mungu aliyemponya yule mtu?”

¹⁸ Nikasema, “La, mama. Mimi si mponyaji. Nina—ninamwomba tu m—mgonjwa, na nilionyeswa na kitu Fulani kilichoniambia.” Sikujua nikiite nini; ono, ama nini. Sikujua kilikuwa ni nini bado. Nilikuwa ni mvulana tu, wala sijaoa na kadhalika. Basi kwa hiyo kulikuwa na... Mama—mama huyu aliniomba niombe, kwa ajili yake. Nami nikamwambia, “Hebu niombe, kwanza, ndipo basi iwapo Bwana atanionyesha nirudi.”

¹⁹ Halafu basi nilipotoka kwenda kuomba... nikakutana na Ndugu George. Basi nikasema, “Huyo ndiye yule mwanamke ambaye ni—nilikuwa nikikwambia kwamba nilikuwa nimeomba kumhusu. Ninajua ni mwanamke yuyo huyo. Andamana nami.”

²⁰ Basi tukaenda huko juu ku—kuomba dua. Na kwa hiyo maskini msichana huyu mwenye umri wa miaka kumi na saba, bila shaka, mimi nikiwa ni mvulana mdogo tu. Naye alikuwa na kaka, yapata umri wa miaka sita, minane, kitu kama hicho. Na kulikuwa na mti wa Krismasi, ilikuwa punde tu baada ya Krismasi, umesimama ndani ya nyumba. Basi wao wakaenda nyuma ya mti huu wa Krismasi, kunicheka. “Kumponya mama yao.” Nilimwambia kwamba Bwana alikuwa anaenda kumponya. Ndipo mimi... Mimi na Ndugu George tukaanza kuomba.

²¹ Basi wakati nilipoanza kuomba, vema, Malaika huyo nimwonaye, Yule ambaye mnamwona kwenye picha, nilimwona amesimama juu ya kitanda. Vema, nilinyosha mkono nikashika mkono wake. Nikasema, “Bibi Ohanian.” Sasa, anaishi New Albany sasa hivi, yeye na mume wake, familia. Basi nikasema, “Bibi Ohanian. Bwana Yesu amenituma, na kuniambia kabla sijaja, ya kwamba, nikuombee, nawe ‘utapona.’ Simama kwa miguu yako, na upate afya, katika Jina la Yesu.” Miguu yake ilikuwa imekunjamana chini yake. Yeye, akiwa na Biblia yake ya Kiarmenia juu ya moyo wake, akaanza kusogea upande mmoja wa kitanda. Na aliposogea, yeye... .

²² Ndipo Shetani akanena nami, kasema, “Acha akanyage hiyo sakafu, atavunjika shingo, kutoka hapo juu kitandani.” Nikahofia kwa muda.

²³ Na mimi siku zote nilikuwa ninajua kwamba hayo maono, sikujua lilikuwa ni nini wakati huo, alikuwa ameniambia daima lilikuwa sahihi. Kwa hiyo nikaendelea, kwa vyovyote vile, nikamwacha atoke kitandani. Naye Mungu akiwa shahidi wangu, mara tu alipoanza, kuruka kutoka kwenye hicho kitanda, miguu yote miwili ikanyoka. Binti yake akapiga mayowe, akivuta nywele zake, na kukimbilia nje mtaani, akipiga mayowe kwa nguvu awezavyo. Majirani wakaja kutoka kila mahali. Naye huyo hapo, kwa mara ya kwanza kwa miaka kumi na saba, akitembea huku na huku katika chumba hicho, akimsifu Mungu. Nikatoka, mara moja, ili niweze kuondokea hilo.

²⁴ Baadaye, nikafahamiana na huyu msichana mdogo, na kuambatana naye. Bila shaka, hili halihitaji kuwa katika kumbukumbu, bali niliambatana na huyo msichana mdogo.

²⁵ Muda si mrefu baadaye, majuma machache, nilikuwa nyumbani mwa mamangu, jioni moja. Nami nilikuwa nikiomba, siku hiyo, ndipo kwa urahisi tu si—sikuonekana kufaulu, kupata u—kupata u—ushindi katika maombi yangu. Basi nikawazia, nitakaa tu ninii yote...mwajua, niende kulala. Nilikuwa nikikaa nyumbani, wakati huo. Na kwa hiyo nikaingia chu—chumbani, ku—kuomba. Na mimi...ilikuwa karibu saa saba usiku, nadhani. Nami ni—nikaomba.

²⁶ Basi, mara ghafla, nilitazama. Na, mama, alizoea kuchukua nguo zake, anazilundika tu kwenye kiti, mwajua. Sisi tulikuwa ni watu maskini sana. Basi nikaangalia, kitu Fulani cheupe kikinijia, nami nikafikiri nilikuwa nikiangalia kile kiti cha nguo. Bali ilikuwa ni yule Malaika wa Bwana, lile—lile Wingu, mwajua. Nalo likaja mahali nilipokuwa.

²⁷ Nami—nami nilikuwa nimesimama kwenye chumba, kidogo, kile tunachokiita nyumba ya “bunduki ya marisaa”, nyumba ndogo iliyonyoka, vyumba viwili ndani yake. Nayo ilikuwa na mbao nyekundu za ukutani hapa juu kwa ajili ya upande huu, mnaona. Kulikuwa na kitanda kidogo cha bango cha chuma upande wangu wa kulia. Kulikuwa na mwanamke mwenye nywele nyeusi amesimama kuegemea...Hicho chumba kimoja kilielekea jikoni. Alikuwa amesimama akiegemea huo mlango wa jiko, akilia. Kulikuwa na baba akisimama karibu nami, na alikuwa ameniletea mtoto, ambaye kitu fulani kilikuwa kwenye maskini kifua chake. Na mmoja, mguu wake wa kushoto, ulikunjamana, mpaka ulikuwa umelalia maskini mwili wake. Nao mguu wa kulia, umekunjamana vingine. Mikono yote miwili imejikunja, pia, kuegemea mwili wake. Nao maskini mwili wake ulikuwa umepindika na kujikunja mpaka ukawa moja kwa moja *hapa* kwenye shingo yake. Nami nikashangaa, “Haya yanamaanisha nini?” Ndipo nikaangalia, ameketi chini upande wangu wa kushoto, na hapo ameketi mwanamke mkongwe, akivua miwani yake, na kuipangusa kutokana na machozi ama kitu fulani kwenye miwani yake. Upande wangu wa kulia, kwenye sofa nyekundu ya kulala, ambayo ilifanana na kiti, aliketi mvulana mdogo, mwenye nywele za rangi ya shaba zenye mawimbi, akiangalia nje kupitia dirishani.

²⁸ Nami nikaangalia, huku amesimama mbali upande wangu wa kulia, na hapa amesimama katika...yule Malaika wa Bwana. Na Yeye akaniambia, “Je, mtoto huyu anaweza kuishi?”

Nami nikasema, “Bwana, sijui.”

Akasema, “Weka mikono yako kumkingama. Ataishi.”

²⁹ Basi ni—nikafanya hivyo. Na mtoto huyo akaruka chini, kutoka kwa...kutoka kwa mikono ya baba yake. Ndipo maskini

mguu wa kulia, ukakunjuka, na upande wa kulia ukakunjuka, mkono wa kulia ukakunjuka. Akaenda hatua nyingine, na upande huo mwingine ukakunjuka. Akaenda hatua nyingine, na upande huo mwingine ukakunjuka, mwili, sehemu ya katikati ikakunjuka. Naye akaweka mikono yake midogo katika yangu, na kusema, “Ndugu Branham, nimepona kabisa.” Mtoto huyo mchanga alikuwa amevaa surupwenye ya kodrai, ama ovaroli, ovaroli ndogo zenye bibu. Na alikuwa na nywele za hudhurungi, na maskini kinywa kidogo, chembamba.

³⁰ Ndipo basi Malaika wa Bwana akaniambia alikuwa ananipeleka mahali pengine. Basi nikapelekwa mbali. Na Yeye akaniketisha chini karibu na eneo la makaburi ya kale, na kunionyesha nambari kwenye jiwe la kaburini, karibu na kanisa. Na Yeye akasema, “Hapa patakuwa mahali pako pa kuelekezea.”

³¹ Akanichukua hadi mahali pengine. Na hapo kulikuwa na . . . palionekana kama palikuwa ni mji mdogo, wenye yapata maduka mawili ndani yake. Na moja lilikuwa manjano upande wa mbele, ubao wa manjano kwenye kuta. Nami nikapanda hapo, ama nikasimama hapo. Na kulikuwa na mtu mkongwe akitoka nje, huku amevaa jaketi la samawati la kodrai, ama jaketi la samawati la jinzi na ovaroli za samawati, pamoja na kofia ya kodrai ya manjano. Alikuwa na masharubu makubwa, meupe.

Akasema, “Yeye atakuonyesha njia.”

³² Na wakati mwingine nilifikia, niliona nilikuwa nikiingia katika chumba fulani, nikimfuata msichana mnene. Ndipo nilipoingia mlangoni, maandishi kwenye karatasi ukutani yalikuwa mekundu. Juu ya mlango kulikuwa na maandishi, “Mungu bariki makao yetu.” Kuna kitanda kikubwa cha kale cha shaba, cha bango, kimewekwa upande wangu wa kulia. Na stovu kubwa imewekwa upande wa kushoto. Na huko katika kona, amelala msichana mwenye umri wa kama miaka kumi na mitano. Naye alikuwa na polio au kitu fulani, ambacho kilikuwa kimeukunja mguu wake wa kulia. Nao wayo wake umeenda kombo, na ukajikunja chini yake. Na yeye—na yeye alionekana kama mvulana. Ila tu, alikuwa na nywele kama msichana, na alikuwa na midomo yenye u—umbo la moyo kama msichana.

Na Yeye akaniambia, “Je, msichana huyo anaweza kutembea?”

Nami nikasema, “Bwana, sijui.”

³³ Akasema, “Nenda ukaweke mikono yako kuingama tumbo lake.” Basi nikafikiri alikuwa mvulana, hakika kabisa, kwa sababu Yeye kunifanya niweke mikono yangu kuingama tumbo lake. Nilifanya kama alivyoniambia.

³⁴ Ndipo nikasikia mtu fulani akisema, “Bwana asifiwe.” Nami nikaangalia juu. Na nilipoangalia juu, msichana huyu alikuwa

anasimama. Na wakati aliposimama, pajama alizokuwa amevaa, mguu wa pajama yake ukajivuta juu, na ukaonyesha goti lenye mviringo kama goti la msichana na si lenye vifundo, mwajua, kama goti la mvulana. Ndipo nikajua alikuwa ni msichana. Naye alikuwa amevaa pajama. Ndipo akaja, akanijia akitembea, akichana nywele zake. Yeye ana nywele zenye rangi ya shaba, akichana nywele zake.

³⁵ Msichana huyo anaishi Salem, siku hizi, ameolewa, na yuna watoto watatu au wanne. Na mama yake na baba wanalipo, pia.

³⁶ Ndipo basi ni—ni—nikafikia. Nami ningeweza kumsikia mtu fulani akisema, “Ndugu Branham. . .” Ama, “Ndugu Bill! Loo, Ndugu Bill!” Naye mama yangu alikuwa akiniita. Ndipo nikawazia. Ningemsikia mmoja, njia moja. Nilitoka kwenye hilo ono, mwajua, kidogo nimedhoofika. Ndipo nikasema, “Unataka nini, mama?” Katika chumba hicho kingine, alipokuwa amelala.

Naye akasema, “Kuna mtu anayebisha mlangoni pako.”

³⁷ Nami nikaisikia, “Ndugu Bill!” Ndipo nikafungua mlango. Kuna mtu aliyeingia. Jina lake John Emil. Anaishi Miami, Florida, sasa. Naye akasema, “Ndugu Bill, hunikumbuki.”

Nikasema, “La. Siamini ninakukumbuka.”

³⁸ Kasema, “Ulinibatiza mimi na familia yangu. Ila,” kasema, “Nilichukua njia isiyo sahihi.” Akasema, “Nilimwua mtu, hapa wakati fulani uliopita. Nilimpiga ngumi, na kuvunja shingo yake, katika mapigano.” Kasema, “Nimempoteza mmoja wa wavulana wangu wadogo, mkubwa zaidi.” Tena kasema, “Mdogo zaidi yuko nyumbani amelala, yuafa sasa.” Tena kasema, “Daktari wa mjini ndiyo kwanza atoke hapa, na kusema, ‘Mtoto huyo ana nimonia maradufu.’ Na anapumua tu kwa shida.” Tena kasema, “Ni—ni—ni—ninaninii tu. . . Ulikuwa moyoni mwangu. Na sijui kama ungekuja na kumwombea.” Tena kasema, “Sasa, kama unavyojua, mimi ni binamu yake Graham Snelling.” Ambapo, Graham Snelling, Kasisi Graham Snelling sasa, alikuwa hajawa mhudumu wakati huo; mvulana mzuri Mkristo. Akasema, “Yeye ni binamu yangu. Ninashuka kwenda kumleta.” Aliyeishi kama nusu maili kutoka kwangu, huko chini jijini. Na akasema, “Ninashuka kwenda kumleta. Nawe utaenda huko?”

Nikasema, “Naam, Bw. Emil, punde tu nitakapovaa nguo zangu.”

Na kwa hiyo akasema, “Nitachukua gari langu, na kukuchukua.”

Nikasema, “Vema.”

³⁹ Kasema, “Punde tu nitakapompata Graham. Nami ninawatakeni nyote mumwombee mtoto huyu.”

Nikasema, “Vema.”

40 Kwa hiyo basi nikaanza kujiandaa. Ndipo mama akasema, “Kulikuwa na nini?”

Nikasema, “Kuna mtoto mchanga anayetakiwa kuponywa.”

Ndipo basi akasema, “Ati kuponywa?”

Nami nikasema, “Naam, mama.”

Na kwa hiyo nikasema, “Nitakwambia zaidi kumhusu nitakaporudi.”

41 Kwa hiyo katika dakika chache, akabisha mlangoni, naye Ndugu Graham alikuwa pamoja naye. Tulikuwa tukienda hapa juu, karibu na kile tunachokijua kama eneo la kuegeshea mashua sasa, ambalo lilikuwa ni maskini Howard Shipyard kwenye wakati huo. Nikasema, “Bw. Emil, hivi wewe... Unaishi wapi sasa?”

Akasema, “Huko juu ya Utica.”

42 Nikasema, “Unaishi katika maskini, kile tunachokiita nyumba ya ‘bunduki ya marisaa’, ya vyumba viwili vidogo.”

“Naam, bwana.”

“Iko juu ya kilima.”

“Naam, bwana,” akasema.

43 Nikasema, “U—ubao wako wa msingi hapa umetengenezwa na ulimi na mtaro nao umepakwa nyekundu.”

Akasema, “Hiyo ni kweli.”

44 Nikasema, “Maskini mtoto mchanga amelala kwenye kitanda cha bango cha chuma. Naye anayo nyumbani, angalau, jozi ya ovaroli ya kodrai ya samawati.”

Anasema, “Ameivaa.”

45 Ndipo nikasema, “Naye mtoto huyo ni jamaa mdogo, yapata umri wa miaka mitatu. Naye pia ana kinywa kidogo chembamba, midomo midogo myembamba. Naye ana nywele za hudhurungi nyepesi.”

Akasema, “Hiyo ni kweli.”

46 Nikasema, “Bibi Emil ni mwanamke mwenye nywele nyeusi. Na katika chumba hiki, una sofa nyekundu ya kulala na kiti chekundu.”

Akasema, “Uliwahi kuwa huko, Ndugu Branham?”

Nikasema, “Muda mfupi tu uliopita.”

“Muda mfupi uliopita?” akasema.

Nikasema, “Naam.”

“Mbona,” akasema, “Sikukuona.”

47 Nikasema, “La. Ilikuwa ni kiroho.” Nikasema, “Bw. Emil, umenisikia nikitaja, nikipabatiza, mambo ambayo hunifanyikia. Hilo huenda... ninaona mambo kabla hayajatukia.”

48 Akasema, “Naam. Je, jambo kama hilo lilikufanyikia, Ndugu Branham?”

49 Nikasema, “Naam. Na Bw. Emil, chochote Hicho kilikuwa kilichoniambia, hakijawahi kuniambia uongo. Mtoto wako ataponywa nifikapo huko.”

50 Ndipo akasimamisha gari, akainama kwenye usukani, kasema, “Mungu, nirehemu. Nirudishe, Ee Bwana.” Mnaona? “Nami ninakuahidi, kukuishia Wewe, siku zangu zote, ikiwa utayaokoa maisha ya mtoto wangu.” Na hapo akatoa moyo wake kwa Kristo. Tukaingia nyumbani, sote tumesisimkwa kumhusu, nafsi kurudishwa kwa Kristo.

51 Wakati sisi—wakati tulipoingia ndani ya nyumba, hapo kila kitu kilikuwa hasa jinsi ilivyokuwa, isipokuwa tu yule mama mkongwe hakuwepo. Kwa msisimko, nimesisimkwa sana, nikasema, “Niletee huyo mtoto.” Naye mtoto karibu amekufa. Unaona? Huko “kukunjamana,” kulikuwa ni uhai kumtoka mtoto huyo. Alikuwa tu amejikunja kufikia *hapa*, maskini koo lake. Ndipo nikasema, “Niletee huyo mtoto.” Bila kungojea ono kutimia.

52 Ndugu Vayle, ikiwa karatasi hii ilipaswa kuwa *hapa*, siwezi kusema chochote mpaka karatasi hiyo iwe hapo. Mnaona? Haina budi kuwa jinsi Hilo lilivyoniyesha.

53 Kwa hiyo nikasema, “Niletee huyo mtoto.” Ndipo baba akaniletea mtoto, nami nikamwombea, na hali yake ikawa mbaya zaidi. Kwa hiyo nikawaza, “Sasa jambo fulani...” Kabisa alikata pumzi, na ilibidi wapambane na kutikisa, na kila kitu, kurudisha pumzi ndani yake. Nikawaza, “Sasa, kuna kasoro fulani.”

54 Ndipo ikatokea nikawazia, “Yuko wapi yule mwanamke mkongwe?” Huyo hakuwepo bado.

55 Kwa hiyo wakamchukua mtoto huyo, wakamlaza chini. Walikuwa wanaweka vitu chini ya pua yake, kadhalika, huku wanalia. Mama yake akipiga mayowe, kwa mfidhaiko, na kadhalika. Lakini mtoto alikuwa anapumua kwa—kwa shida.

56 Nikawaza, “Vema, kupitia u—ujinga wangu, nimetumia vibaya ono la Mungu, maana sikulisubiri, nikiwa nimesisimkwa kupita kiasi.”

57 Kwa hili, unaweza kuona, Ndugu Vayle, ni kwa nini mimi hungojea. Sijali ni nani anayeniambia. Ninakupenda kama ndugu yangu. Ndugu, kamwe usijaribu, kuniambia jambo la kufanya, wakati—wakati ninapojisikia kwamba ni—ninayo mapenzi ya Bwana. Mnaona? Haijalishi linaonekana jema jinsi gani vingine, nitamngojea Yeye. Mnaona? Na—na kwa hiyo ni—nilipata somo papa hapa, miaka mingi, mingi, mingi sana iliyopita; na kufanya hasa kile Yeye asemacho, wala nisilifanye mpaka Yeye anaposema liko tayari kufanywa.

58 Mtoto huyo alikuwa akipumua kwa shida. Sasa, nisingeweza kuwaambia kile nilichofanya, bali ilinibidi tu kungojea. Nikawaza, “Labda neema itaifunika, na Yeye anisamehe.” Vema, nilienda nikaketi chini.

59 Walipigania uhai wa mtoto huyo mpaka mapambazuko. Kulipoanza kupambazuka, walifikiri mtoto huyo angeenda dakika yoyote. Vema, niliketi pale. Nao wakazidi kuniuliza, “Ndugu Branham, tufanye nini?” Ama, “Ndugu Bill,” walivyoniita, “tufanye nini?”

60 Nikasema, “Sijui mimi.” Mnaona? Nikaketi hapo, nimekiinamisha kichwa changu, nikisema, “Bwana, naomba unisamehe.”

61 Vema, ndipo kukapambazuka. Ilibidi Ndugu Graham Snelling aende kazini. Kwa hiyo ilibidi Bw. Emil ampeleke, nami nilijua ilinibidi kutoka humo nyumbani.

62 Na, hata hivyo, Ndugu Graham alipaswa kuwa ameketi hapo, maana ana nywele zenye mawimbi, zenye rangi ya shaba, kama mjuavyo. Alipaswa awe ameketi kwenye sofa hii ya kulala. Kwa hiyo nilikuwa nimeketi hapo ambapo Ndugu Graham alipaswa awe ameketi, ila yule mwanamke mkongwe hakuwepo. Wala hakuna mwanamke mkongwe mahali hapo. Kwa hiyo niliketi hapo. Na kwa hiyo Bw. Emil akavaa koti lake.

63 Ndipo nikajua, kama Ndugu Graham akitoka, ni vigumu kujua wakati atakaporudi. Mnaona? Ndipo basi nikajua, hata akija mwanamke huyo, basi Ndugu Graham hatakuwepo. Kwa hiyo unaona namna ya hali niliyokuwemo.

64 Na hivyo basi Bw. Emil akasema, “Ndugu Branham, unataka kwenda?” Ama, “Ndugu Bill, unataka kwenda nyumbani? Unataka nikupeleke nyumbani?”

65 Nikasema, “La, bwana. Nitangojea tu, ikiwa hutajali.” Nilichukia kukaa hapo kwenye ile nyumba, mtoto peke yake na mama yake, mimi peke yangu, maana walikuwa ni watu wachanga. Wao, mume, alikuwa na yapata umri wa miaka ishirini na mitano, nadhani. Nami nilikuwa na karibu umri uo huo. Ndipo nikasema, “La. Nita—nitangojea tu, ikiwa hutajali.”

Akasema, “Ni sawa, ndugu, Ndugu Bill.”

66 Na kwa hiyo mama akitembeatembea sakafuni, ameshikwa na mfadhaiko, na kujaribu kuninii...akilia na kadhalika, mwajua. Naye mtoto yuko tu mahututi. Mnaona? Ilionekana tu kana kwamba, dakika yoyote, kidogo tu ashikilie pumzi yake, namna *hiyo*, akienda, *anahema*, *anahema*, hiyo tu, ndiyo pumzi, iliyokuwa ndani yake. Wala hakuna kitu...Hawakuwa na penisilini na kadhalika, siku hizo, mnaona. Hivyo basi walininii tu—waliweka tu plasta juu yao, na vitu kama hivyo. Lakini mtoto huyo mchanga alikuwa amekuwa nao kwa siku kadhaa. Naye alikuwa ameenda, mnaona, ama alikuwa yuaenda.

⁶⁷ Ndipo, basi, ni—niliketi chini hapo. Nikawaza, “Jamani, kama Graham akienda...” Graham akavaa koti lake, na akaanza kutoka mlangoni.

⁶⁸ Basi akamwambia mke wake, akasema, “Sasa, tutarudi, hivi punde.”

⁶⁹ Nikawazia, “Ee Mungu, basi itanibidi kukaa hapa siku nzima, na labda usiku kucha, tena, unaona, nikilingojea lile ono. Nifanye nini?”

⁷⁰ Ndipo nikaangalia nje ya dirisha. Na akija kwenye hiyo nyumba, akaja nyanya yake mtoto huyo mchanga. Na, vema, nilikuja kugundua baadaye, alikuwa ni nyanya yake. Naye alikuwa amevaa miwani. Nikawaza, “Hili ndilo, Bwana, ikiwa—ikiwa tu Graham hatatoka nje ya mlango.” Kwa hiyo, huyo nyanya siku zote hutumia mlango wa mbele. Lakini, kwa njia moja ama nyingine, hata hawajui, hadi wa leo, lakini alienda mlango wa nyuma, akaingia jikoni. Basi akatembea jikoni, maskini nyumba hiyo, ya kale. Basi alipofika mlangoni, binti yake akakimbia kule na kumbusu, maana ilikuwa ni mama yake binti, mwajua, na kumbusu. Naye Ndugu Graham...

Kisha akasema, “Je, mtoto amepata nafuu?”

⁷¹ Akasema, “Mama, yuafa.” Ndipo akaanza kupiga mayowe namna hiyo, huku mama yake akilia.

⁷² Ndipo nikawazia, “Hii itafaulu, sasa, ikiwa Graham hatatoka.”

⁷³ Basi nikasimama. Na singeweza kusema chochote, mwaona, kusubiri tu. Basi Ndugu Graham akakaribia. Nilikuwa nimesimama ili naye aketi. Na yeye...Na huyo alikuwa ni jamaa yake, mnaona, kwa hiyo akaanza tu kulia, pia, na kuketi chini kwenye sofa ya kulala ambapo alikuwa awe ameketi.

⁷⁴ Nikawaza, “Sasa, laiti mama huyo mkongwe akaribie tu na kuketi kwenye kiti hiki chekundu!” Ndipo nikarudi mlangoni mahali Bw. Emil alikuwa amesimama, amevaa koti lake kubwa, tayari kuondoka. Hali ya hewa yenye baridi kwelikweli, baridi kama theluji. Basi nikawaza...Ndipo mama huyu mkongwe akaketi kwenye kiti hiki.

⁷⁵ Naye Graham akaketi chini, na kuinamisha kichwa chake chini. Ndipo mama mtoto, akaweka mkono wake juu ya mlango, na kuanza kulia. Sawa kabisa na ono! Naye mama mkongwe akaketi. Na badala ya kuwa ni machozi, kwa jumla, juu ya miwani yake; kutokana na baridi, ilikuwa imeitia ukungu. Ndipo akafungua kijisanduku chake na kutoa lesi ndogo, na, ama mkoba mdogo, akaanza kuipangusa miwani hii. [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] Ndugu, hilo lilitosha.

⁷⁶ Nikamwambia Bw. Emil. Nikasema, “Bw. Emil, ungali una imani nami kama mtumishi wa Kristo?”

Akasema, “Hakika ninakuamini, Ndugu Branham.”

⁷⁷ Nikasema, “Ninaweza kukwambia sasa. Nilinena mbele ya ono, muda mfupi uliopita, hiyo ndiyo sababu halikutendeka. Kama ungali una imani nami, nenda kaniletee mtoto wako mchanga.” Loo, jamani! Ninaona lilikuwa sahihi, basi, mnaona. “Nenda, kaniletee mtoto wako mchanga.”

⁷⁸ Akasema, “Nitafanya chochote utakachoniambia nifanye, Ndugu Bill. Nisingeogopa kumbeba.” Hakika, walipombeba, alienda tu, pumzi ikamwondokea kabisa. Akaniletea mtoto huyo mchanga. Nikanyosha mkono nikamchukua mikononi mwake, nikamvuta kwangu, na kusimama hapo.

⁷⁹ Nikaweka mkono wangu juu yake, nikasema, “Bwana, samehe ujinga wa mtumishi Wako. Unaona? Nilinena mbele ya ono Lako. Bali sasa acha ijulikane kwamba Wewe ni Mungu wa mbingu na nchi.”

⁸⁰ Punde tu, niliposema hivyo, maskini mtoto huyo mchanga akarusha mikono yake yote miwili kumkumbatia baba yake, akaanza kupiga mayowe na kulia, akisema, “Baba, najisikia vizuri sasa.” Mnaona?

⁸¹ Nikasema, “Bw. Emil, achana na huyo mtoto. Itakuwa siku tatu kabla haujamwacha, maana ulifanya hatua tatu, kukunjuka.”

⁸² Nikaenda nyumbani, nikalisimulia katika kanisa langu. Nikasema, “Ninarudi.” Hiyo ilikuwa ni Jumatatu. Nikasema, “Jumatano usiku, kabla ya kanisa, ninaenda huko juu.” Walikuwa ni watu maskini, basi tukawaandalia kikapu cha bidhaa za matumizi nyumbani, kuwapelekea. Hivyo basi nikasema, “Ninawatakeni nyote mwende, wakati nitakapoenda huko. Nanyi mkae nje kuizunguka nyumba. Ndipo nitakapofika mahali hapo, ilipo nyumba hiyo, nyinyi angalieni na mwone kama mtoto huyo mchanga hatatembea sakafuni, akiwa na masharubu meupe yamefanya *hapa*, ambapo amekuwa akinywa maziwa au kitu fulani. Mnaona? Na kuweka mikono yake katika yangu, na kusema maneno haya, ‘Ndugu Bill, nimepona kabisa.’ Maskini mtoto huyu wa miaka mitatu. Chunguza uone kama halitukii.”

⁸³ Mke wangu sasa, Meda, nyuma kabisa kabla hatujaoana, basi alikuwa kwenye hilo kundi. Ndipo watu lori zima wakaenda na kuketi kuzunguka nyumba, unaona, kuniona wakati nikiingia kwa lori kuukuu la Kampuni ya Utumishi wa Umma nililokuwa nalo nyumbani usiku huo. Sikuwa na motokaa yangu mwenyewe. Huku limejaa lami, na kadhalika huko nyuma, mwajua, ambapo nilikuwa nikivuta na kutengeneza vitu, siku hiyo. Nikaendesha hapo mbele, nikasimama. Nikaenda barazani; nikabisha mlango. Nao hawakuwa na mazulia kwenye maskini sakafu hiyo. Basi mama akaja kupitia sakafuni, kasema, “Mbona, ni Ndugu Bill,” namna hiyo. Nao watu

walikuwa wakiangalia kwenye madirisha, wakati huo, kuona kitakachotukia.

⁸⁴ Na katika kona, akicheza, alikuwa ni huyu mvulana mdogo, siku ya tatu. Nikasimama, kamwe sikusema hata neno moja. Ndipo akaja, akitembea kupitia sakafuni, akaweka maskini mikono yake katika yangu. Pamoja na... Alikuwa akinywa maziwa ya chokoleti, maskini masharubu yake, kama, kote *hapo*, kutokana na maziwa ya chokoleti. Akaweka mikono yake katika yangu, kasema, “Ndugu Bill, nimepona kabisa.” Huh!

⁸⁵ Usiku huo, kanisani, nililisimulia. Nikasema, “Kuna msichana kiwete, mahali fulani, aliye mhitaji.” Nikasema, “Kanisa, sijui mambo haya yanamaanisha nini. Siwezi kusema.”

⁸⁶ Na—na kwa hiyo nilikuwa nikifanya kazi kwenye Utumishi wa Umma. Basi ninakumbuka siku moja, yapata juma moja baada ya hapo, nilianza kuondoka kwenye jengo, kwenda nje. Bw. Herb Scott, anayeishi hapa mjini sasa hivi, alikuwa ni bosi wangu. Naye akasema... Nikaanza kushuka. Akasema, “Billy?”

Nikasema, “Naam.”

Kasema, “Kabla hujaondoka, nina barua yako hapa.”

Nikasema, “Sawa, Herbie. Nitaichukua kwa kitambo kidogo.”

⁸⁷ Ndipo—ndipo basi nikaenda kuchukua kazi yangu nyingine, nilikuwa nikikagua. Kwa hiyo nikaenda huko kuhakikisha kazi yangu nyingine imefanywa. Na wakati ni—nilipoenda, nikaikumbuka barua hiyo. Nikaenda na kuichukua, nikaifungua. Na ilisema, “Mpendwa Bw. Branham,” unaona, akasema, “jina langu ni Nail. Mimi ni Bibi Harold Nail. Tunaishi mahali panapoitwa Boston Kusini.” Tena akasema, “Sisi ni Methodisti, kwa imani. Na ilitokea kwamba nilisoma kitabu kidogo ulichoandika, kiitwacho *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*, kijitabu kidogo. Nasi tulikuwa na mkutano wa maombi nyumbani, hivi majuzi usiku. Na sisi tumesikia kuhusu wewe kupata ufanisi, ukiwaombea wagonjwa.” Basi kasema, “Ninaye binti anayeteseka, mwenye umri wa miaka kumi na mitano,” kasema, “ambaye amelala kwenye kitanda cha mateso. Na kwa njia moja ama nyingine, siwezi kabisa kulitoa akilini mwangu, kwamba ninapaswa kukuita uje umwombee msichana huyu. Waweza kumwombee tafadhali? Wako wa kweli, Bibi Harold Nail. Boston Kusini, Indiana.”

Nikasema, “Unajua, huyo ndiye yule msichana. Huyo ndiye.”

⁸⁸ Nikaenda nyumbani, nikamwambia mama yangu, nikawaambia kulihusu. Nikasema, “Huyo—huyo ndiye yule msichana.” Ndipo basi usiku huo, kanisani, nikaliambia kanisa. Nikasema, “Hapa ndipo ma—ma—ma—mahali pale.” Nikasema, “Yeyote anayejua Boston Kusini ilipo?”

⁸⁹ Ndipo Ndugu George Wright, nyinyi nyote mnamfahamu, akasema, “Ndugu Branham, ni...Nafikiri ni huko chini Kusini.”

⁹⁰ Hivyo basi kesho yake, marafiki wangu wawili, pamoja na mke wangu, ambaye sasa ni mke wangu, na mwanamume na mke wake kutoka Texas. Ji-...jina lao lilikuwa Brace, Ad Brace. Anaishi hapa chini sasa, chini ya Milltown, mkulima. Alikuwa mfugaji huko Magharibi. Naye alikuwa amehamia huku ili awe karibu na kanisa. Nami nilikuwa nimemwombea mke wake, naye alikuwa ameponywa ugonjwa wa kifua kikuu. Basi kwa hiyo alitaka kuona huu ukitendeka. Nikasema, “Wewe andamana nami, uone kama hautatukia hivi tu.” Basi mama huyo hakuwa amewahi kuona ono, Bibi—Bibi Brace. Hivyo basi mke wake akaandamana nami. Naye Ndugu Jim Wiseheart, maskini mzee, mnakumbuka, kanisa pale, shemasi mzee, alitaka kuuona. Nilikuwa tu na maskini gari dogo chakavu, la watu wawili wakati huo, nami nikawalundika wote humo ndani.

⁹¹ Na tukateremka chini ya New Albany. Ndipo nikakuta ishara hii, nikaja kugundua, haikuwa Boston ya Kusini. Ilikuwa ni New Boston. Kwa hiyo basi sikujua mahali pa kwenda, basi nikarudi Jeffersonville na kumwuliza mtu fulani. Na mtu fulani akaenda kwenye posta, wakasema, “Boston ya Kusini iko juu ya Henryville.”

⁹² Kwa hiyo ni—nikaenda hadi Henryville, na nikaulizia huko. Nao wakasema, “Geuka uingie barabara *hii*. Ilikuwa yapata maili kumi na tano, kurudi nyuma kwenye vifundo hivi *hapa*, unapata mahali padogo. Utakuwa mwangalifu, usije ukapakosa,” akasema, “kwa sababu ni duka moja dogo tu. Nalo duka hilo lina ofisi ya posta, na kadhalika, ndani yake. Boston ya Kusini, huku kwenye vifundo hivi.” Kuna ekari elfu kumi na saba za hivyo vifundo huko, unaona. Na hii ni nyuma yake, kwenye vilima kule.

⁹³ Kwa hiyo tukaendelea, tukiendesha gari. Ndipo ghafla, nikajihisi nina hali ngeni sana, baada ya kuwa nikiendesha gari, maili tano au sita, nilijihisi kigeni mno. Nikasema, “Sijui.”

Wakasema, “Kuna nini?”

⁹⁴ Nikasema, “Ninaamini kwamba—kwamba Yule ambaye hunena nami, anataka kunizungumzia, kwa hiyo itanibidi kuliacha gari.”

⁹⁵ Basi nikatoka nje ya gari. Nao wanawake wameketi mapajani mwa wanawake, wajua, na kadhalika, lile gari dogo la watu wawili. Ndipo nikatoka nje ya gari, na kuzunguka nyuma ya gari. Basi nikainamisha kichwa changu, nikaweka mguu wangu kwenye bamba, nyuma ya gari. Nami nikasema, “Baba wa Mbinguni, ni nini ungetaka kumjulisha mtumishi Wako?” Na nikaomba. Hakuna kilichotendeka. Nikasubiri dakika chache. Ndipo nikawazia, “Vema, Yeye...” Kwa kawaida palipo

na umati namna hiyo, inanibidi kujitenga. Basi kwa hiyo nikangojea dakika chache.

⁹⁶ Ilitokea kwamba nilivutiwa, kuangalia kule. Ikatokea kwamba niliwazia, “Vema, angalia hapa, hili hapa maskini lile kanisa liko hapa chini.” Na kama ukiwahi kwenye. . . Ni Kanisa la Bunker Hill. Ndipo nikaangalia kando, Kanisa la Kikristo la Bunker Hill, na kulikuwa na mawe ya makaburi ya eneo la makaburini, moja kwa moja mbele ya kanisa.

⁹⁷ Basi nikaenda hapo. Nikasema, “Sasa nyote mnazo barua hizo.” Sikuwa nimewahi kuwa katika nchi hiyo hapo kabla, maishani mwangu. Kamwe sikuwahi kuwa huko juu, popote, maishani mwangu. Ndipo nikasema, “Nyinyi chukueni majina na nambari na mje hapa, mwone kama si ile ile kwenye hili jiwe la kaburini.” Nayo hiyo hapo, hasa kabisa. Nikasema, “Ndiyo hiyo. Tuko kwenye barabara ifaayo sasa.” Nikasema, “Huyo alikuwa ni Malaika wa Bwana.” Mnaona, nilipitia moja kwa moja karibu nalo, wala sikulijua. Kwa hiyo, loo, Yeye ni mkamilifu.

⁹⁸ Na hivyo basi tukaendelea na kuendelea na safari. Moja kwa moja nikakutana na mtu, nami nikasema, “Waweza kunionyesha ilipo Boston ya Kusini, bwana?”

⁹⁹ Akasema, “Nenda pole pole upande wa kulia na kushoto,” wajua, kadhalika namna hiyo. Nasi tukazidi tu kuenda.

¹⁰⁰ Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo, tukaingia, nilitambua, niliingia mahali padogo. Napo palikuwa na namna fulani ya kijiji kidogo, kitu kama hicho. Ndipo ni—nikaangalia. Nikasema, “Hapo ndipo. Hapo ndipo, papo hapo.” Nikasema, “Pale pana. . . Pale, ile pale sehemu ile ya mbele ya duka iliyo manjano.” Nikasema, “Sasa, iweni waangalifu. Mtu atatokea kule, amevaa ovaroli ya samawati, kodrai nyeupe. . . ama kofia ya manjano ya kodrai, akiwa na masharubu meupe, na kuniambia pa kwenda. Kama sivyo, mimi ni mwongo mkubwa.”

¹⁰¹ Na hivyo basi wote walikuwa wanangojea. Ndipo—ndipo nikaendesha motokaa, mbele ya mahali hapo. Na nilipoendelea tu kupanda, mbele, akatokea mtu huyo amevaa suti ya ovaroli ya samawati, na kofia ya manjano ya kodrai, huku ana masharubu meupe. Ndipo Bibi Brace akazimia kwenye gari, akiliona likitimia, namna hiyo.

Nikasema, “Bwana, unapaswa kuniambia mahali alipo Harold Nail.”

Akasema, “Naam, bwana.” Kasema, “Umetoka upande wa Kusini?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

¹⁰² Akasema, “Umepapita. Karibu nusu maili huko chini barabarani, unageuka, barabara ya kwanza upande wa kushoto. Unapanda juu, na utakuta banda kubwa jekundu, basi ingilia

hapo kwenye hilo banda jekundu.” Kasema, “Ni nyumba ya pili mkono wako wa kulia, unapoingia hiyo barabara nyembamba.”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Akasema, “Mbona?”

Nikasema, “Ana binti anayeteseka. Sivyo?”

Kasema, “Naam, bwana. Anaye.”

¹⁰³ Nikasema, “Bwana atamponya.” Ndipo mzee huyo akaanza kulia. Mnaona? Kamwe hakujua. Na kwa hiyo alijumuishwa katika hilo ono. Hakujua kile kilichokuwa kinaendelea.

¹⁰⁴ Nikageuka. Tulimkuta Bibi Nail kidogo amehuishwa tena. Ndipo akaenda huko juu, akatembea uwanjani. Tukatoka kwenye gari, tukaanza kuingia. Tukaanza kutembea mahali hapo kwenye...mwajua, kufikia mahali lilipokuwa. Ndipo msichana mnene akaja mlangoni. Nikasema, “Huyo hapo.” Unaona?

Na kwa hiyo akasema, “Jambo?”

Nami nikasema, “Jambo?” Nikasema, “Mimi—mimi ni Ndugu Bill.”

¹⁰⁵ “Loo,” akasema, “Ni—ni—niliwazia ndiwe.” Akasema, “Ulipata barua yangu?”

Nikasema, “Naam, mama, nilipata.”

Akasema, “Mimi ni Bibi Harold Nail.”

¹⁰⁶ Nikasema, “Vema, nina furaha kukujua, Bibi Nail. Na hili ni kundi dogo tu lililoandamana nami, kumwombea msichana wako.”

Kasema, “Naam.”

Nikasema, “Anaenda kuponywa.”

¹⁰⁷ Akasema, “Ati nini?” Na midomo yake ikaanza kutetemeka. Akaanza kulia.

¹⁰⁸ Nikasema, “Naam, mama.” Na mimi—mimi sijui; sikusimama kwa ajili ya mwanamke huyo.

¹⁰⁹ Nikatembea moja kwa moja sebuleni, huku kundi langu likinifuata. Nilipofungua mlango wa kuingilia sebuleni, nyumba ya mashambani, kubwa, ya kale, nikafungua mlango, hapo palikuwa na magazeti ya manja...ama makaratasi ya manjano ukutani, maandishi mekundu; ishara, “Mungu bariki makao yetu;” maskini kitanda cha bango cha shaba; stovu kubwa imewekwa upande wa kushoto. Na kuna kijitanda kidogo pale, kikiwa na msichana huyu aliyeonekana kama mvulana amekilalia.

¹¹⁰ Sasa jambo fulani lilitukia. Nilikuwa kwenye kona ya chumba hicho, nikitazama mwili wangu ukienda kwenye kitanda hicho. Ndipo nikaweka mkono wangu moja kwa moja kulingama tumbo lake, hasa vile Bwana alivyosema. Ndipo

nilipofanya hivyo, wakati Bibi Nail alipoingia chumbani akaona hilo, huyo akaanguka sakafuni, tena, akazirai. Kidogo yeye ni mtu mnyonge, naye akazirai sakafuni, tena. Basi Ndugu Nail alikuwa akijaribu kumshughulikia. Huku maskini Ndugu Jim amesimama hapo, akisema, “Abarikiwe Bwana,” ameshikilia mikono yake pamoja, laiti nyote mngejua jinsi alivyofanya. Na kwa hiyo basi nikaangalia hilo, nami nikaona hilo.

¹¹¹ Ndipo nikaweka mikono yangu juu yake, ama kusingama tumbo lake, namna *hii*. Nikasema, “Bwana, ninafanya haya kwa amri ya, kile ninachofikiri ni, Mungu akiniambia kuyafanya.” Na yapata wakati huo, akaanza kulia, ndipo akaruka juu.

¹¹² Ndipo wakamsimamisha tu Bibi Nail kwa miguu yake. Alikuwa ameamka, kutoka kwa kipindi chake cha kuzirai.

¹¹³ Ndipo wakati msichana huyo aliporuka kutoka kitandani, huo hapo mguu wa pajama yake ukainuka kwenye mguu wake wa kulia, hasa tu vile ilivyoonekana katika ono. Na hilo hapo goti hilo lililovingirika la msichana, badala ya mvulana.

¹¹⁴ Na hapo Bibi Nail akaanguka, tena. Mnaona? Akazirai. Hiyo ilikuwa ni mara tatu alizokuwa amezirai.

¹¹⁵ Ndipo msichana huyo akatembea kutoka hapo, katika chumba hicho. Akaingia kwenye chumba chake cha kuvalia, akilia, na kuvaa kimono chake, akarudi akitembea, huku akichana nywele zake. Pamoja na ninii yake. . . pamoja na huo u- . . . Na ninii yake—mkono wake mmoja ulipooza, pia, upande wa kulia. Akichana nywele zake kwa mkono huo uliolemaa.

¹¹⁶ Ameolewa, ana watoto kadhaa. Jina lake, sijui jina lake sasa. Lakini la Nail, mtu yeyote angeweza kukwambia, Harold Nail.

¹¹⁷ Na kwamba maono ni kweli. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ningeweza kuwika hilo mahali pake na kukupeleka kwa watu ambao watafanya juzuu la vitabu na mambo kama hayo yametukia. Sasa, hiyo ni kweli, Ndugu Vayle.

¹¹⁸ Nitashindwa; mimi ni mwanadamu. Mimi nimeshindwa, kwa kuanzia, na kabadala duni sana kwa ajili ya mtumishi wa Kristo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹¹⁹ [Ndugu Vayle anasema, “Endeleza Merrell?”—Mh.] M-e-r-r-e, l maradufu. [“Nilifikiri ilikuwa hivyo hapo chini. Naam.”] Ni hayo tu yaliyopo, haya sasa? [“Nail alikuwa N-e-i-l?”] N-a-i-l. [“Brace, B-r-a-c-e?”] B-r-a-c-e, Ad, Ad Brace. [“Sasa nafikiri nimeyataja yote. Hebu kidogo. Graham Snelling?”] Graham, G-r-a-h-a-m. [“Hiyo ni ‘n’ hapo.”] S-n-e, l maradufu, i-n-g. [“Loo, Snelling. Sasa tumelipata.”]



MAONO YA WILLIAM BRANHAM SWA60-0930
(Visions Of William Branham)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa asubuhi, tarehe 30 Septemba, 1960, kwenye Ofisi ya Kampeini huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org